KITABU CHA III

Haki za watoto

# JE, TATHMINI YA MASLAHI BORA NI NINI?



# KARIBU!

## Hadithi hii inahusu vijana wanne — kama wewe.

Wamewasili Ulaya wakiwa salama baada ya safari ndefu.
Vijana wengine waliwasili peke yao. Wengine wao waliwasili wakiwa pamoja na familia.
Wana maswali mengi — na wanasaidiwa na watu wanaofanya kazi mahali wanapoishi.

## Hadithi hii inaweza kukusaidia pia!

**Utajifunza:**

- **Tathmini ya maslahi bora** inamaanisha nini
- unachotarajia
- kwa nini ni muhimu kwako kushiriki na kushirikiana na maafisa hao
- mtu anayeweza kukusaidia
- kuhusu haki zako

**Unaweza kusoma hadithi hii:**

- peke yako
- pamoja na rafiki
- pamoja na mtu anayefanya kazi hapa

## Soma kwa kasi yako. Ni SAWA kusitisha na kuendelea baadaye.

Ikiwa jambo ni gumu kuelewa, **muombe mtu yeyote akueleze**.
Mlezi wako, mfanyakazi wa kijamii au wakili wako wanaweza kukusaidia.

**MWISHONI, UTAPATA:**

- ukurasa wenye taarifa za eneo husika
- maswali ya kufurahisha
- nafasi ya kuandika maswali yako na kuongeza wawasiliani muhimu

Kwa watu walio **chini ya umri wa miaka 18 wanaowasili peke yao**, mlezi atateuliwa. Katika baadhi ya nchi, mlezi pia hujulikana kama mwakilishi.

Pia, katika baadhi ya nchi, **kuomba hifadhi** hujulikana kama **kuomba ulinzi wa kimataifa**.

Mwishowe, tambua kwamba huduma zote zinazotolewa katika vituo vya mapokezi unapoishi hazilipishwi. Ikiwa mfanyakazi atakuomba pesa, zungumza na afisa unayemwamini au mlezi wako.

# **KUTANA NA WAHUSIKA**
# KATIKA HADITHI HII

## Mohamed

Nina umri wa miaka 17. Mimi huwa na furaha wakati mwingi. Ninapenda kuwasaidia marafiki na familia yangu wakati wowote ninapoweza.
Niliwasili peke yangu wiki kadhaa zilizopita na ninamtafuta babu yangu. Nina hamu ya kuanza kufanya kazi.





## Ahmed

Nina umri wa miaka 15. Niliwasili pamoja na dada yangu mkubwa Jasmine, ambaye amekuwa akinilea tangu mama yetu alipofariki. Ninapenda kutagusana na kupata marafiki wapya. Ningependa sana kurudi shuleni haraka iwezekanavyo. Kwa sasa, ninajifunza lugha ya wenyeji wa eneo hili.

## Jasmine

Nina umri wa miaka 24. Niliwasili pamoja na kaka yangu, Ahmed, ambaye ninamlea kadri niwezavyo. Tuliwasili hivi karibuni na tunajaribu kuungana na mjomba wetu ambaye amekuwa akiishi Ulaya kwa muda. Ninapenda michezo na ninacheza vizuri sana mchezo wa mpira ya miguu.



## Adam

Nina umri wa miaka 9. Niko hapa peke yangu. Kwa sasa, nimeamua kutozungumza. Nilikumbwa na mambo mengi mabaya kabla ya kuwasili hapa. Ninahitaji muda kabla ya kuzungumza tena. Lakini mimi ni mwerevu na ninaelewa kila kitu. Mimi ni msikilizaji mzuri sana na ningependa kwenda shuleni. Ninawapenda marafiki wote wapya ambao nimepata kufikia sasa.





## Bint Ines

Mimi ni mlezi anayefanya kazi katika kituo hiki cha mapokezi. Ninajaribu kuwasaidia watoto na vijana wote wanaotafuta hifadhi kadri niwezavyo. Ninapenda kupika na inanifurahisha wakati kila mtu anapokuwa na shughuli za kufanya na kijishughulisha. Mazoezi hutufanya sote tuwe na afya nzuri kimwili na kiakili.

## Bw Fred

Mimi ni mshauri wa kisheria, ambayo ni aina ya wakili. Ninafanya kazi hapa pamoja na wenzangu wengi waliopokea mafunzo mazuri. Ninatoa taarifa na msaada kwa wakimbizi wote wanaoomba hifadhi kuhusu masuala ya kisheria na maombi yao ya hifadhi. Ninapenda kuvaa fulana zenye rangi nyingi zilizo na ujumbe.



Shukrani za dhati ziwaendee kwa wakimbizi wote wanaotafuta hifadhi waliosoma hadithi hii kabla haijachapishwa na kusaidia kuimakamilisha vyema.

Pia walisaidia kuchagua majina ya wahusika wakuu.

Shukrani pia ziendee mamlaka za nchini Malta na Uholanzi zilizowezesha majadiliano na vijana.



BINT INES...
...JE, UNA MUDA KIDOGO ILI UELEZE 'MASLAHI BORA YA MTOTO' INAMAANISHA NINI?
BILA SHAKA! KUMBUKA, MTOTO NI MTU ALIYE CHINI YA UMRI WA MIAKA 18.
NDIYO!
KUZINGATIA MASLAHI BORA YA MTOTO KUNAMAANISHA KUFANYA MAAMUZI BORA NA KUPATA SULUHU BORA ILI MTOTO AWE SALAMA, MWENYE FURAHA NA MWENYE AFYA.
WATU WAZIMA WANAOWALEA WATOTO, KAMA WAZAZI AU MLEZI, DAIMA WANAPASWA KUKUPEA KIPAUMBELE. KILA MTOTO ANASTAHILI KUWA NA MAISHA SALAMA NA YENYE AFYA, CHAKULA, SHULE, MUDA WA KUCHEZA NA FAMILIA YENYE UPENDO.
WATU WANAOKUTUNZA, PAMOJA NA MAMLAKA ZINAZOKUFANYIA MAAMUZI, WANAPASWA PIA KUSIKILIZA MATUMAINI NA HOFU ZAKO.


VIJANA KAMA WEWE WANAOTAFUTA HIFADHI BARANI ULAYA MARA NYINGI HUFIKA WAKIWA PEKE YAO NA WANAHITAJI USAIDIZI.
MLEZI HAJARIBU KUCHUKUA NAFASI YA FAMILIA YAKO BALI ATAKUSAIDIA UKIWA PEKE YAKO. TUNAHAKIKISHA KWAMBA MASLAHI YAKO BORA YANALINDWA HADI PALE UTAKAPOKUWA HUHITAJI TENA MSAADA.
... LAKINI ITAKUAJAE IKIWA MTOTO ANAWASILI AKIWA NA WANAFAMILIA?
MASLAHI BORA YA KILA MTOTO NI MUHIMU. MTU MZIMA YEYOTE ANAYEMLEA MTOTO ANAPASWA KUZINGATIA KILICHO BORA KWA MTOTO HUYO. LAKINI ... SI RAHISI KILA WAKATI. WAKATI MWINGINE WALEZI WANAWEZA KUKUMBWA NA CHANGAMOTO. WAFANYAKAZI WA KIJAMII WALIO MAHALI HAPA WANAWEZA KUWAPA USHAURI.
UNAWEZA PIA KUZUNGUMZA NA MFANYAKAZI WA KIJAMII IKIWA FAMILIA YAKO IMELEMEWA AU HAIKUTUNZI IPASAVYO. MAZUNGUMZO HAYA YOTE YANAHIFADHIWA KWA FARAGHA!


UNAWEZA KUSHIRIKI MAWAZO NA HISIA ZAKO ZOTE NA MLEZI WAKO.
PIA ... MAMLAKA ZINAWEZA KULAZIMIKA KUFANYA MAAMUZI AMBAYO YATAATHIRI MAISHA YAKO. KWA HIYO MLEZI ATAKUSAIDIA KUWASILIANA NAO ILI KUHAKIKISHA KUWA UNASIKILIZWA.
JE, UNAWEZA KUNIPA MFANO WA UAMUZI WANAOHITAJI KUFANYA?
NDIYO BILA SHAKA. MAAMUZI YANAWEZA KUWA NI AINA YA HUDUMA YA MATIBABU UNAYOPASWA KUPOKEA, MAHALI UNAPASWA KUISHI NA NI MTU GANI UNAPASWA KUISHI NAYE.
LAKINI NADHANI NINA UMRI WA KUTOSHA KUFANYA MAAMUZI YANGU MWENYEWE! NATAKA KUWA NA BABU YANGU AMBAYE TULIPOTELEANA WAKATI WA SAFARI YETU.
NINAELEWA. UNAONA, WALEZI WANAKUSIKILIZA.



WANACHUKULIA MAONI YAKO KWA UMUHIMU NA KUSAIDIA MAMLAKA KUELEWA HALI YAKO BINAFSI ... NA KUAMUA KILICHO BORA KWAKO.
WANAFANYAJE HIVYO HASA...?
MAAFISA WALIOPOKEA MAFUNZO WATAKUULIZA MASWALI, ILI KUPATA TAARIFA NYINGI ZAIDI KADRI IWEZEKANAVYO KUHUSU HALI YAKO.
MAJIBU YAKO YATAWASAIDIA KUAMUA KILICHO BORA KWAKO. KATIKA HALI YAKO, AHMED, MAMLAKA KWANZA ZITACHUNGUZA IKIWA BABU YAKO...
... ANA AFYA NJEMA NA NGUVU YA KUTOSHA KUKUTUNZA...
... ANAISHI MAHALI SALAMA...
... ANAWEZA KUKUPA CHAKULA, NGUO NA ELIMU...
... NA AMEKUTENDEA VIZURI KIPINDI CHA HAPO AWALI.


NI KWELI... YOTE HAYA NI MUHIMU!
NDIYO... HII HUEPUKA MATATIZO YA BAADAYE. WAKATI MWINGINE, KILE MTOTO ANACHOTAKA WAKATI WOWOTE HUENDA KISIWE KWA MASLAHI YAKE BORA.
NINAELEWA... MAMLAKA ZINATAKA KUFANYA UAMUZI SAHIHI...
HASWA!
SASA NINAELEWA KWA NINI WALINIULIZA MASWALI MENGI KUHUSU BABU YANGU...
NDIYO, KUULIZA MASWALI MAHUSUSI, HASA WAKATI MAAMUZI MUHIMU YANAHITAJIKA KUFANYWA, **KUNAITWA TATHMINI YA MASLAHI BORA YA MTOTO.**


SHIRIKI TAARIFA NYINGI KADIRI UWEZAVYO.
KUMBUKA, TATHMINI HII INAWEZA KUFANYIKA NYAKATI TOFAUTI, KATIKA MIKUTANO ZAIDI YA MMOJA NA KWA SABABU MBALIMBALI. KATIKA TUKIO LAKO, KWA AJILI YA KUKUUNGANISHA NA MWANAFAMILIA WAKO, INAYOITWA PIA KUUNGANISHWA TENA NA FAMILIA....
... AMBAO NI MCHAKATO WA KUWALETA PAMOJA WANAFAMILIA WALIOTENGANA. JE, UNAWEZA KUFIKIRIA MFANO MWINGINE?
... MTOTO ANAPOISHI MAHALI AMBAPO SIO SALAMA.
HASWA!
UNAMAANISHA NINI UNAPOSEMA 'SI SALAMA'?
KWA BAHATI MBAYA, SI WATOTO WOTE HUWA SALAMA, HASA WANAPOWASILI PEKE YAO.


WATU WENGINE WANAWEZA KUJIFANYA KUWA NI WEMA KISHA WAKUNYANYASE AU WAJARIBU KUKUTUMIA KWA SABABU UKO PEKE YAKO.
WAKATI MWINGINE, HATA WANAFAMILIA WANAWEZA KUWA NDIO WANAOKUNYANYASA.
NI MUHIMU USHIRIKI MAMBO HAYA NA MAAFISA HAO, ILI WAWEZE KUKUSAIDIA.
AFISA ALIYENIULIZA MASWALI ALIKUWA MKARIMU SANA...
NDIYO, MARA NYINGI WAO NI WAFANYAKAZI WA KIJAMII AU WANASAIKOLOJIA WA WATOTO.
HII ILIKUWA YA KUVUTIA NA YENYE MANUFAA. ASANTE SANA!
UNAKARIBISHWA! USIACHE KUULIZA MASWALI!

# MUHIMU

**Katika nchi hii ...**

Mamlaka iliyo hapa inayotoa mahali salama pa kuishi, ambayo pia huitwa **mapokezi**, ni:

______________________________________________________________________

**Ikiwa ningependa kupata melezo zaidi kuhusu:**

- manufaa ya jumla ninayoweza kupewa, kama vile nguo au bidhaa za usafi, ninaweza kuwasiliana au kwenda kwa: ______________________________

- ninachoweza kufanya ninapohisi mgonjwa, ninaweza kuwasiliana na: ______________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

- jinsi ya kwenda shuleni, kujifunza ujuzi au lugha ya wenyeji, naweza kuwasiliana na: ________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Mamlaka inayoshughulikia **ombi** langu la **hifadhi** ni: ______________________________
______________________________________________________________________

Jina la mlezi wangu ni: ______________________________________________
______________________________________________________________________

Ikiwa nina nia ya kujifunza zaidi kuhusu **tathmini ya maslahi bora**, wakati inapofanyika na kinachotokea na taarifa ninazoshiriki, naweza kuzungumza na mlezi wangu au nitazame:

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

# MUHIMU

**Katika nchi hii ...**

Ninaweza pia kuwasiliana na mshauri wa kisheria bila malipo ili kujifunza zaidi kuhusu utaratibu wa kuomba hifadhi na mada zinazohusiana. Kwa hili, ninaweza kuwasiliana na: ______________________
______________________________________________________________________

Ikiwa mtu yeyote anayefanya kazi hapa, kama maafisa, washauri wa kisheria, wafanyakazi wa kijamii au mlezi wangu, wananitendea vibaya, ninaweza kuwasilisha malalamiko na kuwasiliana na: ________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

Iwapo kutatokea dharura, ninaweza kuwasiliana na huduma za ambulensi kwa
______________________________________________________________________
au polisi kwa ______________________________________________________________

Taarifa nyingine muhimu: ____________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

# MASWALI

**Ninatathmini ujuzi wangu kuhusu kile nilichojifunza kuhusu tathmini ya maslahi bora.**

Chagua majibu sahihi.

1 Kuzingatia maslahi bora ya mtoto kunamaanisha...

- ○ a. Mamlaka hunisikiliza mimi na mlezi wangu ili kuelewa hisia zangu, mahitaji na maoni yangu, ili waweze kufanya maamuzi yaliyo bora kwangu.
- ○ b. Hakuna mtu atakayenisikiliza.

2 Ili kujifunza kuhusu mahitaji yangu na kile kinachonifaa zaidi katika hali mahususi, mamlaka yataniuliza maswali wakati wa tathmini ya maslahi bora.

- ○ a. Kweli
- ○ b. Sio kweli

3 Je, ni kwa nini mamlaka hufanya tathmini ya maslahi bora?

- ○ a. Ili kupata suluhu bora kwa ajili yangu wakati maamuzi muhimu yanapohitajika kufanywa, kama vile ni wapi ninapaswa kuishi na mtu yupi.
- ○ b. Kwa sababu wanapenda kuzungumza.

4 Maslahi bora ya mtoto ni muhimu tu kwa watoto wanaowasili bila wazazi.

- ○ a. Kweli
- ○ b. Sio kweli

5 Maafisa wanaofanya kazi mahali ninapoishi watawasiliana nami na mlezi wangu mara kwa mara ikiwa nina mahitaji yoyote mapya.

- ○ a. Kweli
- ○ b. Sio kweli

## Majibu ya maswali

Swali la 1: a Swali la 2: a Swali la 3: a Swali la 4: b Swali la 5: a

# MADOKEZO

## SWAHILI

Kijitabu hiki kinakusudiwa kutoa taarifa pekee. Hakiundi kivyake haki au wajibu wowote. Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi (EUAA) limetoa sehemu kuu ya nyenzo hii, na kunakili na kufanya mabadiliko kwa kijitabu hiki kumeidhinishwa na EUAA pekee kwa Nchi Wanachama wa EU. EUAA haikubali jukumu au dhima yoyote ya usahihi, maudhui, ukamilifu, uhalali au kutegemeka kwa taarifa zilizojumuishwa katika kijitabu hiki na Nchi Wanachama wa EU au na mhusika mwingine yeyote anayewajibika. EUAA wala mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya EUAA hawajibikii matumizi yoyote yanayoweza kutokana na taarifa zilizomo katika kijitabu hiki.

© Shirika la Umoja wa Ulaya wa Masuala ya Hifadhi, 2025

